

Kuandikishawa kwa elimu ya mapema

Wazazi wapendwa na walezi wa kisheria!

Umejulishwa yakwamba mtoto wako amepatikana kuwa na ulemavu wa kusikia. Hakika utakuwa na maswali mengi sasa kuhusu nini cha kutarawa kwako na familia yako:

Je! Unaweza kufanya nini sasa?

Nini kifuatacho?

Unawezaje kumsaidia mtoto wako?

Je! Ni misaada gani ya kusikia inayofaa mtoto wako?

Je! Lugha ya ishara itamsaidia mtoto wako kiviipi?

Je! Unaweza kupata msaada gani?

Je! Ni tiba gani ambazo ni muhimu na zinazo mfaa mtoto wako?

Je! Mtoto wako anaweza kuhudhuria shule gani baadaye?

Ili tuweze kuyajibu maswala haya na mengine mengi tuna huduma inayozingatia msaada wa elimu ya mapema ya watoto walio na ulemavu wa kusikia. Kupitia njia hii, tungependa kukusaidia kupata majibu ya maswali yako. Mwalimu kutoka timu yetu ya msaada wa mapema atafanya ufadhili wa mapema pamoja na wewe nyumbani kwako. Ikiwa mtoto wako bado anatembelea shule ya chekechea, msaada wa mapema waweza fanyika hapo shuleni mwake. Lakini mawasiliano kati yako kama mzazi na mwalimu wako wa elimu maalum bado ni muhimu sana!

Nani anapata msaada wa mapema wa ufundishaji?

Watoto wote, watoto wachanga na watoto wa chekechea walio na ulemavu wa kusikia.

Ni vyema kupata ufadhili na usaidizi wa mapema mtoto akiwa na umri wa angalau miezi mitatu na bado hajaenda shule. Ni muhimu sana kuanza kujifunza mapema! Watoto ambao wana ulemavu mwingine wanaweza pia kupata usaidizi wa mapema.

Je! Msaada wa mapema hufanyika mara ngapi?

Watoto wengi hupokea lisali limoja la usaidizi wa elimu ya mapema mara moja kwa wiki.

Wakati mwingine msaada wa elimu ya mapema hufanyika tu kila wiki ya pili. Hii inaweza kuwa na manufaa kwa watoto, kwa mfano, ambao tayari wana miadi mingine mingi. Hakuna usaidizi wa mapema wakati wa likizo za shule na likizo za sikukuu shuleni kwetu.

Ninawezaje kupata msaada wa mapema kwa mtoto wangu?

Matoleo yote ya ufadhili wa mapema hayahitaji malipo kutoka kwako. Pia hauhitaji kichocheo kutoka kwa daktari wako au kliniki. Ni wewe tu kama mzazi au mlezi wa kisheria unaweza kuomba usaidizi wa elimu ya mapema. Swala hili linahitaji hatua tatu:

Hatua ya 1:

Tafadhali wasiliana na Kituo cha Ushauri:

Bi Antje Suppelt

Simu: 02151 - 65 60 8-124

Barua pepe: antje.suppelt@lvr.de

Hatua ya 2:

Tunaweka miadi ya mashauriano katika kituo cha ushauri.

Mashauriano huchukua kama lisali limoja.

Tafadhali usisahau kuleta yafuatayo kwa ushauri:

- mtoto wako
- Kitabu cha ulemavu wa mtoto wako (*U-Heft*).
- Barua za daktari kutoka kwa daktari wa mtoto wako au mtaalam wa sauti na maskio ya watoto.

Hatua ya 3:

Wakati wa mashauriano, unatia sahihi kwa ombi la usaidizi wa mapema.

Ikiwa unaishi katika Rhein-Kreis Neuss, itabidi uwasilishe mtoto wako tena katika idara yako ya afya baada ya ushauri. Hii haihitajiki kwa maeneo mengine yoyote ya makazi isipokua Rhein-Kreis Neuss.

Ombi lako la usaidizi wa mapema litatumwa moja kwa moja kutoka kwa kituo cha ushauri. Baada ya takriban wiki tatu, mwalimu wako wa kibinafsi wa elimu ya mapema atawasiliana nawe. Kisha mnaweza kufanya kazi pamoja ili kupata miadi inayofaa pande zote mbili.

Je, una maswali zaidi?

Kisha tafadhali wasiliana nasi. Tunakutarajia!